

**SUBSIDIARY LEGISLATION**

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 25 Vol. 89 dated 20<sup>th</sup> June, 2008  
 Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 83 la tarehe 20/6/2008

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**  
**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 6 (1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KUEGESHA MAGARI) ZA HALMASHAURI YA  
 MANISPAA YA MOROGORO, 2008.

- |  |           |
|--|-----------|
| 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kuegesha Magari) za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, 2008 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.  | Jina      |
| 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika kwenye eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.   | Matumizi  |
| 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakavyoelezwa vinginevyo:<br>"Afisa mwidhinishwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia Sheria Ndogo hizi;<br>"Halmashauri" ina maana ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro;<br>"Kituo cha basi" maana yake ni kituo kilichoidhinishwa na Halmashauri ambapo mabasi yanayotoa huduma ya usafiri kwa umma, hupakia na kushusha abiria;<br>"Maagesho yaliyotengwa" maana yake ni sehemu yaliyotengwa maalum ya kuegesha gari; | Ufafanuzi |

